Utah State Board of Education

# Bodi ya Elimu ya Jimbo la Utah

Fomu ya Ridhaa ya Wazazi kuhusu Mafunzo ya Elimu ya Ngono

***Wazazi wanapaswa kupokea fomu hii ndani ya kipindi kisichozidi wiki mbili kabla ya kuanza kwa mafunzo***

Tarehe ya/za Mafunzo Yaliyopangwa: ____________________________________

Jina la Mwanafunzi:________________________________________________________________

Kozi:_______________________________________Mwalimu/Walimu:_____________________________

Shule:______________________________________Nambari ya Simu:______________________

Mzazi Mpendwa,_______________________________________________________

Kama sehemu ya elimu ya mtoto wako, amejiunga kwenye kozi yenye mafunzo kuhusu mada zinazohusiana na elimu ya ngono. Umepewa fomu hii ya ridhaa kwa sababu mafunzo na/au majadiliano ya mada za elimu ya ngono yanadhibitiwa na sheria ya jimbo na kanuni ya Bodi ya Elimu ya Jimbo la Utah. Tafadhali soma fomu kwa makini, chagua **chaguo moja**, utie sahihi, na umrudishie mwalimu aliyetajwa hapo juu. Mwanafunzi wako hataruhusiwa kushiriki katika shughuli za darasani bila fomu hii iliyojazwa na kutiwa sahihi kuwasilishwa.

**<u>Maelezo</u>**

Mafunzo yote yanayohusiana na elimu ya ngono yataendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Jimbo la Utah State (53G-10-402) na kanuni ya Bodi ya Elimu ya Jimbo la Utah (R277-474) kama ifuatavyo:

- Shule inahakikisha kuwa mafunzo yanasisitiza umuhimu wa kutoshiriki katika shughuli zote za ngono kabla ya ndoa na kuwa mwaminifu baada ya ndoa.
- Kutakuwa na ridhaa ya awali kutoka kwa wazazi kabla ya kufundisha maudhui yoyote ya elimu ya ngono kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya Utah 53G-10-403.
- Nyenzo za mpango huu na wageni wanenaji wanaotoa mafunzo ya mada hizi wamekaguliwa na kuidhinishwa na kamati ya elimu ya eneo (LEA) ya ukaguzi wa nyenzo za mtaala.

Maudhui yafuatayo HAYAJAIDHINISHWA na Bodi ya Elimu ya Jimbo kwa ajili ya mafunzo na hayatafundishwa:

- Maelezo ya kina ya tendo la kujamiiana, kuamsha hamu ya ngono, au mwenendo wa kimahaba;
- Utetezi wa shughuli za ngono kabla ya ndoa au nje ya ndoa;
- Utetezi au uhamasishaji wa matumizi ya njia au vifaa vya kupanga uzazi; na
- Njia au mbinu zozote zinazowezesha au kuhamasisha ukiukaji wa sheria yoyote ya jinai ya serikali ya jimbo au ya serikali kuu na mtoto au mtu mzima, ikiwa ni pamoja na kujibu swali la ghafla kutoka kwa mwanafunzi.

Utah State Board of Education

Kulingana na Kanuni R277-474-7-4, walimu wanaweza kujibu maswali ya wanafunzi au kusahihisha kauli zisizo sahihi mradi tu majibu yao yazingatie sheria ya serikali ya jimbo na nyenzo kufundishia zilizoidhinishwa. Walimu pia wanaweza kuwaelekeza wanafunzi kwa wazazi.

Mtaala wa kozi hii unajumuisha mafunzo au majadiliano kuhusu mada zilizowekewa tiki hapo chini. (*Kwa Matumizi ya Mwalimu Pekee)*:

- ☐ Uidhinishaji kwa mujibu wa 53G-10-404
- ☐ Magonjwa sugu, ya kuambukiza, na makali na hali ya mfumo wa uzazi, ikiwa ni pamoja na maambukizi na magonjwa ya zinaa (STI, STD).
- ☐ Taarifa kuhusu mbinu au vifaa vya kupanga uzazi
- ☐ Mbinu bora za uchumba, ndoa, na uzazi, kwa mujibu wa mfuatano wa mafanikio kama ulivyofafanuliwa katika 53G-10-402
- ☐ Ukuaji wa binadamu, ikiwa ni pamoja na kubalehe na kukomaa
- ☐ Anatomia na fiziolojia ya mfumo wa uzazi wa binadamu
- ☐ Mchakato wa uzazi wa binadamu, ikiwa ni pamoja na utungaji mimba, ukuaji wa kijusi, ujauzito, na kujifungua
- ☐ Ujuzi wa kukataa kama ulivyofafanuliwa katika 53G-10-402
- ☐ Kutoshiriki Ngono

Maonyesho ya jinsi ya kutumia njia, mbinu au vifaa za kupanga uzazi **yamepigwa marufuku**

**<u>Machaguo ya Mzazi: Tafadhali soma na weka tiki mojawapo tu katika ya Yafuatayo:</u>**

**Jina la Mwanafunzi**: ____________________________________________________

☐ **Chaguo la 1** Naruhusu mtoto wangu kushiriki kwenye majadiliano husika kama ilivyoelezwa hapo juu.

☐ **Chaguo la 2** Naruhusu mtoto wangu kushiriki kwenye majadiliano husika kama ilivyoelezwa hapo juu, isipokuwa ____________________________________. Naelewa kwamba mtoto wangu atapewa kazi mbadala ya darasani yenye kiwango sawa na hatashiriki somo hili lililo kwenye ratiba ya kawaida katika siku ya mafunzo haya. Naelewa kwamba mtoto wangu atapewa sehemu iliyo salama na yenye uangalizi ndani ya shule wakati wa somo hili. Itakuwa ni wajbu wake kuripoti kwenye sehemu hii iliyotengwa awali, kujitambulisha kwa mwalimu au msimamizi, na kuwasilisha kazi iliyokamilika ya darasani kwa mtu sahihi.

☐ **Chaguo la 3** Kabla ya kuamua, nitawasiliana nawe shuleni ndani ya wiki mbili zijazo ili kupanga wakati wa kujadili mtaala uliopangwa na kuhakiki nyenzo

☐ **Chaguo la 4** SIRUHUSU mtoto wangu kushiriki katika majadiliano yoyote kama yalivyoonyeshwa kwenye kisanduku hapo juu. Ninaelewa kuwa mtoto wangu hahusiki katika sehemu isiyo la lazima ya mtaala. Badala yake atapewa mahali salama, panaposimamiwa ndani ya shule wakati wa darasa, na atapokea kazi mbadala inayohusiana na vipengele vingine vya kozi.

Fomu hii ya ridhaa inapaswa kutumwa kwa wazazi kwa muda usiozidi wiki mbili kabla ya mafunzo ya mada iliyobainishwa. Kwa mujibu wa sheria ya jimbo, mtoto wako hawezi kushiriki shughuli ya mafunzo iliyo kwenye ratiba na iliyoainishwa hapo juu isipokuwa na baada ya barua hii ya ruhusa

iliyosainiwa irudishwe kwa mwalimu aliyebainishwa kwenye fomu hii. Fomu zilizosainiwa zitahifadhiwa kwenye faili hapa shuleni kwa kipindi kisichopungua miaka miwili.

Tafadhali tia sahihi na urudishe fomu hii ili kuthibitisha umeikagua na kuchagua chaguo moja kutoka kwenye orodha iliyo hapo juu.

**Saini ya Mzazi/Mlezi: ______________________________________________**

**Nambari ya Simu:__________________________Tarehe:_________________**